# Mkakati wa Vyama vya Wafanyakazi katika kupambana na Virusi vya Ugonjwa wa Ebola (VUE) 2014 -2016

***OCTOBER 2014***

**Utangulizi**

Mlipuko wa Virusi vya Ugonjwa wa EBOLA (VUE) katika nchi za Afrika ya Mashariki ni janga kubwa la kibinadamu ambalo limeonesha udhaifu uliomo ndani ya mifumo ya utoaji wa huduma za afya katika nchi husika. Udhaifu uliojionesha katika mifumo ya huduma za afya katika nchi za Liberia, Guinea na Sierra Leone umekuwa na athari katika nchi za jirani na hata nchi nyingine zilizopo mbali zaidi, kwamba maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola (VUE) na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo, umejitokeza hata Marekani na Hispania.

Hadi kufikia mwisho wa wiki ya tatu ya mwezi Oktoba mwaka 2014, kulishakuwa na vifo vya watu ambao idadi yao inakaribia 5,000 kutokana na VUE, ingawa upo uwezekano kuwa idadi hiyo ikawa kubwa zaidi. Balaa hili linatisha zaidi kutokana na ukweli kwamba ilipofikia tarehe 19 ya mwezi Oktoba mwaka 2014, wahudumu wa Afya 416 waliambukizwa na virusi vya ugonjwa wa Ebola (VUE) kutokana na kuwahudumia wagonjwa wenye maambukizi ya Ebola. Wahudumu wa Afya 244 ambao waliambukizwa virusi vya ugonjwa huu, wamefariki. Kwa maneno mengine ni kwamba asilimia tano (5%) ya watu ambao wanajulikana kuambukizwa na kufariki kutokana na virusi vya ugonjwa wa Ebola katika nchi za Guinea, Liberia na Sierra Leone ni wafanyakazi watoao huduma katika sekta ya afya.[1]

Vifo vya wafanyakazi wa sekta ya afya kimsingi vimesababishwa na mazingira mabovu ya kazi , upungufu wa vifaa vya kinga kwa wahudumu, upungufu wa mazingira salama ya kazi, miundombinu hafifu, idadi ya wahudumu kuwa ndogo na hivyo kulazimika kuwa muda mrefu karibu na wagonjwa, na hakika kutotosheleza kwa rasilimali kumepunguza uwezo wa kupambana na maambukizo haya. PSI inazo taarifa kwamba wafanyakazi wa sekta ya afya waliokufa, hawakuwa na kinga ya kutosha kutoka mifumo ya hifadhi ya jamii, na matokeo yake familia zao zimeachwa katika umasikini mkubwa.

Kukosekana kwa usalama kwa hivi sasa ni tishio. Zipo taarifa kuwa wafanyakazi wa sekta ya afya wanaojihusisha na uhamasishaji dhidi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola hushambuliwa na hata kuuwawa (kama vile ilivyowahi kutokea kwa wale wafanyakazi wa afya waliohamasisha matumizi ya kinga dhidi ya ugonjwa wa polio).

**Maudhui**

Vyama washirika wa PSI vilianza mwezi Aprili, 2014 kutoa taarifa za wafanyakazi wanaokufa kutokana na kuwahudumia wagonjwa walioathirika na virusi vya ugonjwa wa Ebola. Wamekuwa wakitoa taarifa hizo hata kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Afya wa nchi za Afrika ya Magharibi uliofanyika mjini Monrovia mwezi huo wa Aprili, 2014. Mwezi Julai, mwaka 2014 Vyama Washirika wa PSI wa mtandao wa Vyama vya Wafanyakazi wa sekta ya Afya wa Afrika ya Magharibi (WAHSUN) walitamka waziwazi kuwa vyama hivyo vinayo nafasi muhimu katika kuuandaa mfumo wa huduma za afya kwenye matukio ya dharura kama haya ya mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa Ebola. Inasikitisha kukumbuka kuwa tahadhari zote kutoka kwa Vyama hivi vya Wafanyakazi, kwa kiwango kikubwa, zilipuuzwa Mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa sekta ya afya katika nchi za Afrika ya Magharibi kabla y mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa Ebola (VUE) yalidhihirisha hali mbaya ya mifumo ya huduma za afya katika nchi hizo;

---

[1]World Health Organization (WHO) **Ebola Response Roadmap: Situation Report** 22 October 2014http://ow.ly/Dh6Qraccessed 23 Oct 2014

mazingira yasiyoridhisha, rasilimali zisizotosheleza mahitaji, huduma zisizotosha na wahudumu waliozidiwa na kazi. Shirika la Kazi Duniani (ILO) linakadiria kuwa mfumo wa huduma za afya unaotosha unapaswa kuwa na wahudumu wa afya 41 kwa idadi ya watu 10,000, lakini hali halisi katika nchi zifuatazo siyo ya kuridhisha kama ifuatavyo.[2]

- Guinea 2/10.000
- Liberia 3/10.000
- Nigeria 20/10.000
- Senegal 5/10.000
- DRCongo 4/10.000

Kwa hiyo hali mbaya tunayoishuhudia kutokana na mlipuko wa VUE, kwa ujumla wake, ni dalili na matokeo ya kukosekana kwa uwekezaji wa kutosha kwenye sekta na mifumo ya afya kwa miongo mingi, na kwa nchi za Liberia na Sierra Leone, baada ya vita na vurugu, hazikuchukuliwa hatua za kutosha kuikarabati miundo mbinu ya mifumo ya huduma za afya.

Kwa hakika hatua za haraka zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa Ebola ni zile zinazohusu urekebishaji wa miundombinu ya sekta ya afya kama vile kuhamasisha upatikanaji wa msaada kutoka nchi za nje kutoa rasilimali kuijenga miundombinu n.k. Lakini hatua zozote zile zinazochukuliwa haziwezi kutatua matatizo ya muda mrefu ya kisiasa ambayo ndiyo yamesababisha mifumo ya afya ya Umma kuharibika, kukosekana kwa mazingira nadhifu ya kazi na haki za wafanyakazi kutozingatiwa ipasavyo katika kukabiliana na majanga makubwa ya afya.

## Mkakati wa Vyama vya wafanyakazo

Vyama vya Wafanyakazi vinapaswa kuweka mkakati wa kukabiliana na changamoto hii. Ni muhimu kwa sasa hivi kuwa tatizo la kisiasa linalojitokeza, liwekwe wazi. PSI ndiyo ipo katika nafasi nzuri ya kusimamia masilahi ya kisiasa siyo tu ya wafanyakazi wa sekta ya afya na Vyama vya Wafanyakazi, bali pia jamii yote ambayo inayo haki ya kuwa na mfumo bora wa afya. PSI, na washirika wake ni waelewa wa kile kinachohitajika katika mfumo bora wa afya ya jamii.

Mkakati wa Vyama vya Wafanyakazi, wakati huu ni lazima utambue kuna kuwa, nafasi yao siyo ile ya:-

1. Kutoa misaada ya ukarimu
2. Kuchukua nafasi ya Serikali.

PSI ni lazima itambue kuwa nafasi yake siyo ile ya Wakala wa Ustawi wa Jamii, ingawa zipo sababu nyingi na za kutosha za kutoa misaada ya dharura kwa wanachama wa Chama cha Wafanyakazi pindi ikibidi. Gharama za misaada hiyo zinaweza kuwa kubwa mno ambazo PSI – haina uwezo wa kugharamia.

Lakini PSI haipaswi pia kujiingiza katika mambo ambayo ni wajibu wa Serikali kuyatekeleza. Wajibu wetu ni kudai ili Serikali itekeleze wajibu wake wa kusimamia utoaji wa huduma bora za afya, na wala siyo wajibu wa PSI kuziba mapengo yale ambayo Serikali inashindwa kutekeleza wajibu huo. Zipo sababu za kawaida na za kisiasa. Kwa hali halisi, wanachama wetu wanaweza kujikuta katika mazingira ya hatari, mfano Chama cha Wafanyakazi hakiwezi kujiamulia jinsi na namna ya kugawa misaada, au kuamua ni makundi gani ya jamii yaelimishwe na uhamasishaji kuhusu Ebola. Kisiasa tungekuwa tunazihujumu hoja zetu wenyewe kuhusu mifumo ya utoaji huduma bora kwa jamii, na wala hatupaswi kuuingiza mfumo wa utoaji huduma za afya kwenye utaratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, na tuepuke kuuweka mfumo huo chini ya makampuni ya kibiashara hata kama ni kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na mashirika hayo.

Nguvu ya PSI haipo kwenye uwezo wa kifedha wa wanachama wake lakini ipo kwenye ushirikiano na utendaji wa pamoja unaotupatia uwezo wa kijamii kusikika, kuhamasisha na kuleta mabadiliko ya maendeleo. Huu ndiyo uwe ni mfumo wetu wa utendaji katika masuala ya

[1]World Health Organization (WHO) **Ebola Response Roadmaesponsertage of skilled health workers, by country**http://ow.ly/Dh73Saccessed 2 Oct 2014. No data for Sierra Leone was available.

kupambana na virusi vya ugonjwa wa Ebola na harakati zetu za kujitahidi kuujenga upya mfumo wa utoaji huduma ya afya ya jamii katika Afrika ya Magharibi.

**Utekelezaji**

Katika mazingira haya PSI lazima iwe na malengo ya aina mbili katika ngazi tatu (ya taifa, kanda, na dunia). Lengo la kwanza kabisa ni kuvisaidia Vyama vya Wafanyakazi katika kudai mazingira na hali bora za kazi katika sekta ya afya na wafanyakazi wake katika nchi za Afrika ya Magharibi. Lengo la pili lina sehemu mbili:-

- Kuendeleza nafasi ya Vyama kama wahusika katika hatua zote za kupanga harakati za mapambano dhidi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola.

- Kufanya kampeni za uhamasishaji ili kuboresha na kupanua mifumo ya utoaji wa huduma za afya katika nchi za Afrika ya Magharibi.

Rasimu ya jedwali la mkakati wa utekelezaji na maelezo yake unafuata hapa chini. PSI itahitaji kuwa na kundi la wawakilishi wanaofanya kazi Afrika ili kuutekeleza mkakati huu. Kundi hili linapaswa kuwa na wawakilishi wafuatao:-

- Wawakilishi katika nchi za Guinea, Sierra Leone, Liberia na DRC, ambao wataendesha shughuli katika ngazi ya taifa.
- Wawakilishi wa asasi za kanda (hasa wa ILO na ECOWAS, - wakiwa na ofisi Abuja, Nigeria).
- Mratibu wa eneo wa kuratibu kazi zote, mwenye ofisi ACCRA, Ghana.

PSI inatarajia kujitafutia fedha kwa ajili ya shughuli hii.

Tunapoamua kuanzisha programu mpya kwa ajili ya Afrika ya Magharibi, lazima tujipime na kutambua nguvu zetu na upungufu wetu katika mazingira ya sasa. Katika nchi za Guinea, Liberia na Sierra Leone Vyama vya Wafanyakazi vinavyowawakilisha wafanyakazi watoao huduma za afya, ni dhaifu (kutokana na mazingira yao, ukandamizaji na matatizo ya ndani ya vyama hivyo), PSI inapaswa kuvijengea uwezo vyama hivyo ili vishiriki katika kutekeleza malengo ya kuboresha mazingira ya kazi ya wafanyakazi hao. Kwa upande mwingine Vyama vya Wafanyakazi wa huduma ya afya katika nchi za Nigeria na Ghana vina nguvu zaidi. Kwa hiyo PSI iviombe Vyama hivi kushiriki katika programu hii.

Vile vile yapo mambo mengi muhimu ya kujifunza kutoka nchi za Senegal, Nigeria na DRC. Katikati ya mwezi wa Oktoba Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza kuwa Senegal na Nigeria hazikuathirika na Virusi vya Ugonjwa wa Ebola (VUE).[3] Hapa lazima tuone ni kwa kiasi gani Vyama vya Wafanyakazi katika nchi hizo vilishiriki na kama kuna uzoefu wowote ulipatikana ambao nchi nyingine zinaweza kuutumia. Katika DRC mlipuko wa ugonjwa wa Ebola unaonekana kutohusika na milipuko ya nchi nyingine, lakini kule kuna washirika imara wenye uzoefu wa kufanya kazi na PSI.

Mwisho kabisa, ni vema tukatahadharisha kuhusu uwezekano wa kuendeleza zoezi hili. Lazima tujiridhishe kuwa Vyama vya nchi hizo zote zitakuwa na uwezo wa kuendesha programu hii bila msaada kutoka nje baada ya mwaka 2016? Hili ni suala la tahadhari tu ingawa halipo katika malengo ya sasa hivi, na si vema kutarajia kuona matokeo katika kipindi kifupi. Tunachopendekeza hapo ni kuona kuwa hatua za haraka zinachukuliwa ili kukabiliana na janga la virusi vya ugonjwa wa Ebola, ni baada ya mwaka 2016 ndipo tutakapoweza kufanya tathmini ili kuona kama malengo tuliyojiwekea ni endelevu.

**Hitimisho**

Ingawa mamilioni na hata mabilioni ya dola na yuro zinasakwa na kuahidiwa kupatikana kwa ajili ya Afrika ya Magharini, hatupaswi kutarajia kwamba mifumo ya utoaji wa huduma za afya Afrika ya Magharibi, itabadilika mara moja.

---

[3]**WHO declares end of Ebola outbreak in Nigeria**http://ow.ly/DhaCx Accessed 23 October 2014; **The outbreak of Ebola virus disease in Senegal is over**http://ow.ly/DhbJP Accessed 23 October 2014

Lakini tuna imani kuwa Vyama vya Wafanyakazi vinao uwezo mkubwa kwa kuwashirikisha wanachama wetu kujihusisha katika michakato ya maamuzi katika kukabiliana na janga hili. Hakika tunayo nafasi kubwa katika kuleta hali bora ya mifumo ya utoaji wa afya, kuvijengea vyama vya Wafanyakazi uwezo wa kuboresha mazingira ya kazi ya wafanyakazi na sekta ya afya wote.

Matarajio ya PSI ni kuona kuwa itakapofika mwisho wa mwaka 2016, Vyama washirika vyote vitakuwa vinaendesha kampeni na kujenga mahusiano ya kuweza kufikia malengo ya programu hii. Mwisho, tutambue kuwa tunayo fursa ya kuubadili mwelekeo na mijadala ya kuendeleza mifumo ya afya. Mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa Ebola hudhihirisha ni kwa jinsi gani jamii yoyote inaweza kudhurika kutokana na kukosekana kwa mifumo bora ya afya ya jamii.

**RASIMU - Jedwali la Mkakati wa PSI wa jinsi ya Vyama vya wafanyakazi Vitakavyopambana na Virusi vya Ugonjwa wa Ebola (VUE ) mwaka 2014 - 16**

Mapambano ya Awali: Guinea, Liberia, Sierra Leone, Democratic Republic of Congo (DRC)
Mapambano ya Awamu ya Pili: Ghana, Nigeria

| Lengo | Matokeo Tarajiwa | Viashiria | Muda | Shughuli |
|---|---|---|---|---|
| Afya na Usalama sehemu ya kazi (DHS) na mazingira ya afya za wahudumu kuboreshwsa katika nchi zenye virusi vya ugonjwa wa Ebola. | Vyama vya Wafanyakazi kukamilisha mapendekezo kuhusu Afya na Usalama Kazini na mazingira bora ya kazi ya wahudumu wa afya katika ngazi ya kanda, na taifa.<br><br>Vyama kuzihamasisha Serikali zao na mashirika ya kanda, na mataifa kuyakubali mapendekezo hayo.<br><br>Kupatikana mikataba na makubaliano kati ya Vyama na Serikali.<br><br>Vyama kuwatambua watu na kuwaandaa wenye uwezo wa kuendesha kampeni dhidi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola. | Vyama vimetambua mahitaji ya programu.<br><br>Vyama vimeyaainisha maeneo ya kuboresha mazingira ya kazi (muda wa kazi, uwiano wa wahudumu na wagonjwa, zamu za kazi) na mabadiliko yanayohitajika katika hatari sehemu za kazi.<br><br>Vyama vimeainisha mapendekezo ya kuboresha hifadhi ya jamii na mazingira ya kazi.<br><br>Unions have begun campaigns on unified proposals.<br><br>Vyama kuendesha kampeni za pamoja kuhusu mapendekezo yao.<br><br>Wawakilishi wa PSI – WAHSUN kuanza kazi Guinea, Liberia, Sierra Leone, na ofisi za Mratibu Kanda ya Ghana, Accra. | TBC | Kuandaa madodoso ya programu.<br><br>Kufanya utafiti wa kitaifa kuhusu Afya na Usalama Kazini, hifadhi ya jamii na mazingira ya kazi.<br><br>Kufanya makongomano ya kitaifa kuhusu Afya na Usalama Kazini.<br><br>Kufanya makongomano kuhusu hifadhi ya jamii na mazingira ya kazi.<br><br>Kufanya tathmini ya shughuli katika ngazi ya kanda. |
| | | | | |
| Kuvishirikisha Vyama vya Wafanyakazi wa huduma za afya katika michakato ya kuandaa sera na mipango kwenye ngazi za kitaifa na kanda, kuhusu:-<br><br>1. Jinsi ya kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola katika nchi za Afrika ya Magharibi na DRC.<br><br>2. Kuboresha na kupanua mifumo ya utoaji wa huduma za afya ya jamii katika nchi za Africa Magharibi na DRC. | PSI na Vyama vya Wafanyakazi katika sekta za afya katika nchi zenye mlipuko wa ugonjwa wa Ebola kushirikiana na kutoa taarifa za pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, ya kijamii na ya jumuia.<br><br>PSI na Vyama vya Wafanyakazi katika nchi zenye mlipuko wa ugonjwa wa Ebola Afrika Magharibi na DRC, kuendesha kampeni za pamoja katika ngazi za taifa, kanda na kimataifa ili kuchukua hatua stahili dhidi ya virusi vya ugonjwa wa Ebola, na kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma za afya. | Vyama vimeainisha mapendekezo ya kitaifa na kikanda kwa ajili ya maendeleo ya mfumo wa huduma za afya.<br><br>Vyama vimeainisha na kuorodhesha mashirika yasiyo ya kiserikali ya kijamii na jumuiya, ya kushirikiana nayo katika nchi za Afrika Magharibi.<br><br>PSI na Vyama vimefanikiwa kuzishawishi serikali za nchi, mashirika ya kikanda na ya kimataifa ((WAHO, ECOWAS, WHO, ILO, WB, IMF) na kufanikiwa kupatikana kwa maamuzi ya mipango ya muda mrefu na ya muda mfupi.<br><br>PSI kufanikisha makubaliano na mashirika ya fedha ya kimataifa (IFLs, kuhusu sera na shughuli zao (AFDB, IMF, WB). | TBC | Kufanya utafiti kuhusu mifumo ya utoaji wa huduma za afya ya jamii katika ngazi ya taifa.<br><br>Kufanya utafiti kuhusu mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kijamii na ya jumuiya<br><br>Makongomano ya kitaifa, kanda na kimataifa kwa kushirikiana na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kijamii na ya kijumuiya.<br>Ushawishi wa mashirika ya taifa kuhusu uboreshaji wa mifumo ya afya kutoka ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. |